# Shaykh Ali Hasan Al-Halabi Aijibu Kauli ya Shaykh Muhammad Bin Sa'eed Raslaan Dhidi Yake

# [Prt 2]

8 February, 2014 | Posted by Salafibayaan | Refutations | 373 views

Mfasiri: Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad.

Ndio Ewe Dr Raslân, haya ni makala yangu.

Sasa ni wapi ambapo ujumbe wako muhimu unapoeleza 'upotofu' wangu?

Si mbali, muda mchache uliopita, nilikuwa nikitizama utovu wa adabu mpya wa daktari wa tiba, Muhammad Bin Sa'îd Raslân, namuombea Allâh amuongoze katika radhi zake, ambao ulikuwa ni jawabu la makala yangu jana. Daktari huyu, namuombea Allâh amsamehe, akauita kama 'ujumbe mpya kwa Halabi'. Ndani yake akanisukuma nimjibu, kwahivyo hapa nipo nafanya hivyo, kwahiyo usipande hasira!

Maneno yake mapya **hata hayakuzidi** dakika nane na nikang'ang'ana kutafuta ndani yake 'ilmu yoyote au fiqhi za kujadili! Kwa hakika, kutokana na ninayoyakumbuka, maneno yake hayana Qur'ân, istilahi za kisheriya wala riwaya za kutoka kwa Salaf isipokuwa kwa hadîth moja tu, ambayo amedanganya kudai kuwa mimi siijui! Haliyakuwa makala yangu juu yake yamebeba âyât, ahâdîth, maneno ya Salaf, maneno ya wanavyuoni na mas'ala mengine ya kimsingi ya 'ilmu.

Licha ya yote hayo, Raslân, Allâh amuongoze, aliyapa nyongo, huku akibuni lugha ya kushawishi lakini safari hii kwa njia mpya.

Sasa kufanyejwe? Maneno yake, ambayo ni matupu yasiyo na 'ilmu yoyote wala ukweli, ni ya ukosefu wa adabu mtupu yenye kuonyesha mambo mawili katika wakati mmoja, uwoga na ujinga!

Ni dhahiri kwa kila aliye na macho, au miwani (!), yakwamba daktari, kama inavyo-onekana, amekasirika na kuhamaki, hata kama alikuwa akijaribu kuficha hayo, lakini hakuweza kufanya hivyo! Ama kuhusu uwoga wa Raslân, basi kule *ku-Sabb* (kulaani) kwake, ambako ni kitendo kinachofanana na jina la mtaa wake anakotoka *"Subk"*, kisha akayafanya maneno yake kama mashairi utadhani ni *Maqâmât* ya *Badî' uz-Zamân* au *Maqâmât* ya *Harîrî*!

Isipokuwa utamkuta Raslân akiwa amejificha nyuma ya maneno kama vile, "baadhi yao wanasema", au "baadhi yao wanadai", "timu moja yasema", na "timu nyengine yasema" – Raslân alikuwa akiyasema yote hayo ili apate kusema kuhusu lolote analotapika apate kisingizio kuwa "haya si maneno yangu". Lau kama utakuwa ni mwenye kuyawacha baadhi ya maneno yake, utadhani kuwa alikuwa akizungumzia kuhusu timu hii na timu ile za mpira, kama timu ya Al-Ahly na Zamalek!

Ewe Raslân, uko wapi ujasiri wako wa fasihi, na watuwiye radhi watu wa fasihi, katika kujieleza kuhusu uliyonayo ndani yako waziwazi, kama ufanyavyo kwa kawaida na lugha zako chafu, za ujeuri na istihzai kwa yoyote mwenye kukukosoa, ukiwagoa kuhusu makomo yao, mijitumbo, nywele zao, na hata jinsi walivyozaliwa na mama zao?! Allâh na amrehemu mmojawapo wa Salaf aliyesema **"Sisi twahitaji zaidi kiyasi kidogo tu cha adabu kuliko tunavyohitaji 'ilmu nyingi".**

Hii ni "jawabu yangu muhimu" kwa mmojawapo wa ndugu aliyekerwa na baadhi ya maneno makali katika makala yangu ya kwanza.

Sasa wewe daktari Raslân, kwa masikitiko hutoweza kufaidika kabisa kutokamana na niliyoandika mwishoni mwa makala yangu ya kwanza ambayo yalikuwa na msingi wa ki-ilimu, Manhajiyyah, uwazi, kweupe na ya moja kwa moja. Sasa mimi nakwambia wewe, "Njoo na dalili za huwo "upotofu", "viini" au "takfiri", na wala usijilete na maneno matupu yasiyokuwa na chochote."

Lakini sisi hatukuona lolote katika maneno yako mapya, ambayo yasiyokuwa na tafauti yoyote na ya zamani, ambayo bado yanarudia ukosefu wa adabu uleule kuhusu viini, vyoo, sehemu za siri, wanawake wenye kucheza dansi na umalaya wa kitaalamu, na maneno mengine ya ufafanuzi yenye kumuweka mbali na Akhera. Pasi na kuyataja matamshi ya Raslân yaliyo mbali na jawabu za ki-'ilmu, ambayo mimi naweza kusema kwa uhakika yakwamba hatutoyaona kwa njia yoyote, kutokana na (viini!), Manhaj ya ghuluw na tajrîh, ambazo viongozi wao walifaulu kukuburuta na kukuingiza wewe na wakakutumia haliyakuwa wewe hukutambua! Kama wanavyokuchukulia wewe katika kuwafaidisha wao katika mabishano haya, wameona yakwamba wewe umeyakubali haya, na haya yote ewe Raslân ni kujiridhisha nafsi yako na "*kitumbo nge"* wako wa karibu atakaefichuliwa, bila ya shaka, pamoja na uchafu wake.

Mimi nimekurubia kuweza kusema yakwamba hata kama ungeliweza, ewe Raslân, kuleta chcochote ambacho mimi niliombwa nilete, wewe hutoweza kuleta chochote. Hiyo ni kwa sababu mambo yote na mengi yake ambayo *ma-Ghulât* wanayojaribu kukosoa nayo, ambayo wao vilevile waliyokutushia wewe kukufanyia, yanajulikana, yameshafichuliwa na kupatilizwa! Ujinga wao umetatiwa na taqlîd zao zimegunduliwa kujaa matatizo.

Kwahivyo Raslân hawezi kuja na jambo lolote jipya baada ya miaka hii mitano, ambayo tayari tushayakosoa. Katika wakati huu ujinga wao umetushughulisha sisi, na katika wakati ambao wewe umekuwa ukikosoa yaliyotokea Misri kutokana na kufuatilia mapinduzi, kisha yakaja mapinduzi baada ya mapinduzi!

Miongoni mwa sababu za daktari kumulikwa ni katika yaliyomshtua yeye kutokana na idadi ya watu kusomwa ambayo makala yangu ya kwanza yaliyopata kwenye ukumbi wetu kulalsalafiyeen, ambayo mpaka kufikia leo ba'dal Asr yamefikiya zaidi ya 10,000, licha ya pua zao. [Mpaka sasa hivi idadi imepanda mpaka 16,000!] kutokana na haya, ewe Raslân, zaidi ya mmoja wa *ma-Shayâtîn* kutoka katika wana-adamu na majini, sio *"Kitumbo nge"* umpendaye tu peke yake, wamekusukuma ukimbilie kunijibu!

Jawabu lako, Raslân lilikuwa ni nyororo kama "taarifa ya habari" kutoka katika shirika la utangazaji la al-Jazîrah au al-'Arabiyyah, hili lilifanya kwa kutafuta suluhisho kwa *Jumu'ah*, ingawa muda wa maisha ya mtu uko katika milki ya Allâh, kabla ya kundi la watu waovu kutoka kwa wafuasi wake, iwapo ni kubwa au ndogo, waliyasikiya hayo!

Ewe daktari Raslân, mimi naweza, bila ya kujigamba, kukukosoa juu ya kila neno moja la urongo ulilolisema kwa maneno kumi zaidi!

Na ninao uwezo, wa kukugeukia wewe juu ya kila matamshi ya kijinga uliyoyatoa.

Yako wapi majibu yako kuhusu niliyoyasema hapo awali, au hata kuhusu baadhi ya niliyoyasema hapo awali? *Wallâhi* wewe hata si hodari kuliko huyo Ibn Hâdi!

Ref: http://kulalsalafiyeen.com/vb/showthread.php?t=55762
Posted by Abdul Kareem Ibn Ozzie